

Serikali kutoa bei elekezi maziwa

Na Lulu George, TANGA

SERIKALI imeahidi kuharakisha utoaji wa bei elekezi ya maziwa ili wafugaji wanufaike tofauti na sasa.

Pia, imesema kuna mikakati ya kuongeza thamani ya zao hilo ili kuleta ushindani wa ubora katika soko la ndani na nje ya nchi.

Ahadi hiyo ilitolewa na Naibu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini, Charles Malunde, katika mahojiano na Nipashe, baada ya kikao kazi kilichoshirikisha vyama vya msingi vya ushirika mkoani humo kwa uratibu wa Chama Kikuu cha ushirika wa wafugaji mkoani Tanga (TDCU).

Aliwataka wafugaji kuachana na ufugaji wa mazoea na kufanya wa kisasa ambao utakuwa na tija kwa maendeleo yao binafsi na kwa maslahi ya taifa.

Bei ya maziwa mkoani Tanga ni Sh. 1,200 kwa lita moja huku pakiti moja yenye ujazo wa milimita 250 (sawa na robo lita) yanayotoka viwandani yakiuzwa kwa Sh. 600.

Malunde alisema licha ya bei iliyopo kulalamikiwa na wafugaji wengi, inaweza kumpa faida ndogo hasa kwa mfugaji ambaye atatumia mbinu bora na za kisasa za kilimo

ikiwamo kuongeza lishe, mitamba yenye ubora na kuhakikisha anaongeza uzalishaji wa maziwa kila siku.

"Katika hili lazima tuelewane, haiwezekani mfugaji huwalishi ng'ombe wako kama inavyotakiwa, unazalisha lita tati za maziwa kwa siku, mitamba yenyewe unachukua ya mtaani tu halafu utegemee maziwa yakupe faida hilo litakuwa ndoto," alisema.

"Hata kama serikali itapandisha bei ya maziwa, lakini hutaweza kutumia bidhaa hiyo kujiletea maendeleo utaona kwamba biashara haina faida," alisema.

Alisema upo mpango uliowekwa kwa wafugaji kupitia vyama vyao vikuu vya ushirika kuwakopesha mitamba bora ya kisasa kwa utaratibu wa kukusanya kiwango fulani cha maziwa kila siku kama malipo ya mitamba hiyo watakopa.

"Kuna utaratibu umewekwa kupitia vyama vikuu vya ushirika ambapo mfugaji ataweza kupeleka maziwa lita tano kila siku, ikiwa ni fidia ya malipo ya mkopo wa mtamba atakaokopeshwa kwa mujibu wa makubaliano watakayowekeana hivyo wafugaji wachangamikie fursa hiyo," alifafanua.

The Guardian pg. 3, Tuesday

15/12/2020

* 9 veterinary physicians given stern warnings *

By Guardian Reporter

NINE veterinary physicians from different district councils have been given stern warnings for non-submission of reports on livestock diseases to the responsible authorities, whilst 10 others were given one-week to submit their reports.

Speaking at the weekend on the sidelines of the 38th Tanzania Veterinary Association (TVA) conference held in Arusha from December 10 to 12, this year, the Veterinary Council of Tanzania (VCT) Registrar Dr Bedan Masuruli said nine veterinarians are required, in a period of one

year, to submit their reports to the Livestock Services Department under the Ministry of Livestock and Fisheries on a weekly and monthly basis.

Dr Masuruli explained that on December 9, this year the Council convened an emergency meeting to discuss claims on various veterinary experts who have failed to submit weekly and monthly reports of veterinary diseases to the Livestock Services Department whereby about 40 per cent of the experts out of 184 local councils do not do so.

He said 78 experts were not submitting reports, however after initial interrogation, 34 experts

were discovered not to have submitted their reports at all, and the Council, at the meeting summoned veterinary experts from various local councils, whereas 19 responded to the summons.

He said during interrogation, 10 veterinary experts who said they had evidence of reports submitted were given one week to give the evidence.

He said the nine others who did not have any evidence of reports submitted were given stern warnings and to ensure that in the coming one-year they should not fail to submit both weekly and monthly reports on livestock

diseases.

The VCT Registrar said the council, in collaboration with the Livestock Services Department, will continue to provide training to veterinary experts on the importance of submitting reports on livestock diseases from their local councils.

Livestock Services Department under the Ministry of Livestock and Fisheries has been receiving both weekly and monthly reports on livestock diseases to enable the ministry to assess the situation of livestock diseases in the various areas of the country for appropriate action to eradicate the diseases.